



Maelezo ya Haraka Kuhusu Kuandikisha Upya Medicaid, Child Health Plus, au Bima ya Afya ya Essential Plan

Je, wewe au mwanafamilia kwa sasa ana bima ya afya kupitia New York State Medicaid, Child Health Plus au Essential Plan?

Kuanzia Msimu wa Kuchipua wa 2023, Jimbo la New York hivi karibuni litaanzisha upya ukaguzi wa ustahiki ili kuhakikisha kwamba wasajiliwa bado wanastahili kwa mipango hii. Hii imaanisha unaweza kuhitaji kuchukua hatua ili kuandikisha upya bima yako ya afya au bima ya wanafamilia wako. Kwa mfano, ikiwa mapato yako yamebadilika sana kuanzia kabla ya janga la COVID-19 kuanza, inawezekana kwamba unaweza kuhitaji kuripoti taarifa hiyo kwa NY State of Health ili kuendelea kusajiliwa katika bima ya afya.

Haya ni baadhi ya mambo unayoweza kufanya sasa ili kujiandaa:

1 Jisajili kwa arifa za ujumbe.

Jisajili kupokea arifa za ujumbe kutoka kwa NY State of Health ili usikose taarifa muhimu kuhusu bima ya afya, ikiwa ni pamoja na wakati wa kuandikisha upya bima yako. Ili kujisajili, **tuma ujumbe wa neno START kwa 1-866-988-0327.**

2 Hakikisha kwamba anwani yako imesasishwa.

Hakikisha kwamba NY State of Health au ofisi ya Medicaid ya eneo lako ina anwani yako ya sasa ya barua, nambari ya simu na anwani ya barua pepe ili waweze kuwasiliana nawe kuhusu bima yako ya afya.

Ikiwa una bima katika NY State of Health, unaweza:

- Piga simu kwa 1-855-355-5777 (TTY: 1-800-662-1220)
- Ingia katika akaunti yako kupitia nystateofhealth.ny.gov
- Kupata msaidizi katika <https://info.nystateofhealth.ny.gov/findassistor>

Ikiwa una Medicaid **kupitia kwa ofisi ya Medicaid ya kaunti yako au kupitia New York City's Human Resources Administration (HRA)**, wasiliana na ofisi ya eneo lako utoe anwani yako na maelezo yako ya mawasiliano.

3 Chukua Hatua.

Inapofika wakati wa kuandikisha upya bima yako ya afya, utapokea barua kutoka NY State of Health au kifurushi cha kuandikisha upya ikiwa ulijiandikisha kupitia ofisi ya Medicaid ya kaunti yako. Barua/kifurushi hiki kitakujulisha unachohitaji kufanya ili kuandikisha upya bima yako na muda unaopaswa kujibu. Fuata maagizo sasa hivi.

Ili kuendelea kupata taarifa na maelezo zaidi tembelea: <https://info.nystateofhealth.ny.gov/COVID-19-Changes>

NY State of Health ni Soko Rasmi la Mpango wa Afya la New York.

Kwa usaidizi wa kuandikisha upya bima yako na kupata maelezo kuhusu tarehe ya kuandikisha upya:

📞 **Tupigie simu kwa :
1-855-355-5777 au
TTY: 1-800-662-1220**

AU

📧 **Wasiliana na msaidizi karibu nawe kwa: <https://info.nystateofhealth.ny.gov/findassistor>**

AU

📍 **Wasiliana na ofisi ya Medicaid katika eneo lako kwa: https://www.health.ny.gov/health_care/medicaid/ldss.htm**

NY State of Health inafuata sheria za haki za raia za Taifa na sheria za jimbo zinazotumika, na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, jinsia, umri, asili ya kitaifa, imani/dini, hali ya ndoa/familia, rekodi ya kukamatwa, hatia ya(za) jinai, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mwathiriwa wa unyanyasaji wa nyumbani na/au kulipiza kisasi.